

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'

Simu Na. 027-2530022

Barua

pepe:ded@hanangdc.go.tz

Tovuti:www.hanangdc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
Halmashauri ya Wilaya ya Hanang',  
2 Barabara ya Amani,  
S.L.P. 2,  
27382 Ganana – Hanang',  
MANYARA.

TANGAZO LA ZABUNI


TANGAZO LA ZABUNI YA UWAKALA WA UKUSANYAJI WA USHURU WA  
MAZAO YA CHAKULA, BIASHARA NA MISITU  
ZABUNI NA.LGA/059/2023/2024/NC/01

Tarehe: 26/04/2023

**KWA: WAZABUNI**

1. Mwaliko huu wa Zabuni unafuatia Tangazo la Jumla la Ununuzi kwa ajili ya **Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 lililotangazwa katika mfumo wa Kitaifa wa Ununuzi kwa njia ya Mtandao (TANePS).
2. Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' inapenda kualika zabuni kutoka kwa watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa ukusanyaji wa Ushuru wa mazao ya Chakula, Biashara na Misitu kutuma maombi yao kwa Zabuni hii.
3. Ushuru wa Mazao ya Chakula, Biashara na Misitu utahusu kukusanya ushuru wa Mahindi, Maharage, Ngano, Alizeti, Kartamu, vitunguu, mbaazi, ulezi, mkaa, mbao, nta na mazao mengine yanayouzwa katika Tarafa za Katesh, Endasak, Simbay, Bassotu na Balangdalalu. Ushuru wa mazao ya Chakula, Biashara na Misitu hautahusisha mazao ya mashamba makubwa ya wawekezaji ambayo ni Gidagamowd, Setchet, Murjanda, Mulbadaw na Bassotu Plantation.

4. Mwombaji asiwe Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang au Mheshimiwa Diwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang au Mfanyabiashara ya mazao ya chakula, Biashara na misitu
5. Unaalikwa kuwasilisha Zabuni yako kwa ajili ya kukusanya **Ushuru wa Mazao ya Chakula, Biashara na Misitu** kama ilivyoainishwa kwenye Nyaraka za Zabuni.
6. Zabuni zote zikiwa zimejazwa kikamilifu zivasilishwe Halmashauri ya Wilaya Hanang' kupitia TANEPS kabla ya **saa 5:00 asubuhi tarehe 11/05/2023** Ufunguzi wa Zabuni hizo utafanyika kupitia TANEPS mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilishwa Zabuni katika tovuti: [www.taneps.go.tz](http://www.taneps.go.tz) .
7. Zabuni au sehemu za Zabuni ambazo zitawasilishwa kwa njia nyingine tofauti na TANEPS au zilizowasilishwa katika muundo usiokubalika na TANEPS, hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini, bila kujali mazingira yoyote.



Ibrahim E. Mbogo

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'  
MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA  
HANANG**